NEW

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA

**Tarehe:** 25 Septemba, 2023

# TANGAZO LA MIKOPO KWA WATUMISHI

Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga imepata mgawo wa fedha za Mfuko wa Mikopo kwa Mwezi Septemba, 2023 shilingi 350,000,000 na kuelekezwa kuwa maombi ya mkopo yawasilishwe Hazina kwa kuzingatia mgao uliotolewa. Imeelekezwa kuwa vigezo vyote vya kutoa mikopo vizingatiwe kama ilivyoelekezwa katika Waraka wa Watumishi Na. 3 wa Mwaka 2011, ikisomwa pamoja na rekebisho namba "C" la Waraka wa Watumishi wa Serikali Namba 3 la Mwaka 2011.

**Masharti ya mkopo ni kama ifuatavyo:**

i. Watumishi watakaokopeshwa ni wale wanaobaki na theluthi moja (1/3) ya mishahara yao baada ya makato yote.

ii. Watumishi ambao hawatakuwa na mikopo mingine watafikiriwa kwanza.

iii. Mtumishi anayehitaji kukopeshwa aandike barua kwa Mkurugenzi kupitia kwa Mkuu wa Idara/Kitengo husika.

iv. Mtumishi haruhusiwi kukopeshwa mkopo mwingine wa fedha za kununulia magari, samani na matengenezo ya magari na pikipiki hadi atakapokuwa amemaliza kulipa mkopo wa awali.

v. Mtumishi ataruhusiwa kukamilisha taratibu za maombi kwa njia ya mtandao baada ya kuchaguliwa kupitia uchambuzi utakaoratibiwa na Kamati ya Mikopo ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga.

vii. Viwango vya mkopo kwa watumishi na muda wa marejesho:

# VIWANGO VIPYA VYA MIKOPO YA FEDHA TASLIMU

| AINA YA MKOPO | NGAZI YA MSHAHARA | KIWANGO CHA JUU CHA MKOPO KINACHOPENDEKEZWA (TSHS) | MUDA WA MAREJESHO |
|---|---|---|---|
| Mkopo wa fedha taslimu kwa ajili ya ununuzi wa magari, pikipiki, samani na matengenezo ya vyombo vya usafiri. | TGS A-C, TGTS A-C, TGHS A-C, AGCS 1-2, TJS 1-2, TGOS A-C, TGHOS A-C, SAIS A-C | 15,000,000.00 | Miezi 72 |
| | TGS D-F, TGTS D-F, TGHS D-F, AGCS 3-4, TJS 3-5, TGRS A-C, SAIS D-F | 30,000,000.00 | Miezi 72 |
| | TGS G-H, TGTS G-H, TGHS G-H, AGCS 5-6, TJS 6, TGTS D-E, SAIS G-H | 40,000.000.00 | Miezi 72 |
| | LESSE 1-4, TGTS I, TGHS I-J, AGCS 7-9, TJS 7-9, TGRS F-1, SAIS I-K | 50,000,000.00 | Miezi 72 |
| | LSSE 5-9, TGHS K-L, AGCS 10-12, TJS 10-12, SAIS L-Q | 55,000,000.00 | Miezi 72 |

**JINSI YA KUTUMA MAOMBI YA MKOPO:**

Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kupitia masjala bayana zikiwa pamoja na nakala ya hati ya mshahara ya sasa (Current Salary Slip). Fomu za maombi ya mkopo zitajazwa kwa njia ya mtandao baada ya kuidhinishwa kukopa.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 02/10/2023 saa 09.30 alasiri.

Mwl. Alexius R. Kagunze

**MKURUGENZI WA MANISPAA**

MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
SHINYANGA

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa, 20 Barabara ya Mwanza, Mtaa wa Chamaguha, S.L.P.28, 37182 Shinyanga.

Simu:028-2763213, Barua pepe: md@shinyangamc.go.tz, tovuti: www.shinyangamc.go.tz